

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

Simu: 025-2540035/7

Barua pepe: [ded@kyeladc.go.tz](mailto:ded@kyeladc.go.tz)

Nukushi: 025-2540425



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

S. L. P. 320, **KYELA,**  
**MBEYA - TANZANIA**

**Tarehe 16.08.2017**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa kushirikiana na program ya Walter Reed, anatangaza nafasi za kazi ya Karani wa Takwimu (Data Clerk) nafasi nne (4).

### SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe ni Mtanzania asiyepungua umri wa miaka 18 na asiyezidi umri wa miaka 45.
2. Awe amehitimu mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
3. Mwenye sifa ya Astashahada, Stashahada, na Shahada ya Teknolojia ya habari; Sayansi ya Komputa ni sifa ya ziada.
4. Awe na uzoefu usiopungua miezi sita kazini.
5. Awe mwaminifu na mtunza siri.

### MAJUKUMU

1. Kuhakikisha kumbukumbu za wateja wa CTC zinatunzwa kulingana na mwongozo wa taifa.
2. Kuingiza taarifa za wateja kwenye Mfumo wa Kielektroniki, kila siku.
3. Kusaidiana na watoa huduma za Afya, katika kuandaa taarifa ya kila mwezi, robo na mwaka.
4. Kutoa taarifa za wateja wasiofika kwa wakati kupata huduma, kila mwezi na kurekodi mrejesho kulingana na muongozo.
5. Kufanya uchunguzi (Data Quality Check) wa taarifa zinazoingia kwenye mfumo wa taarifa kabla na baada ya kutunza kumbukumbu kwa siku husika.
6. Kushirikiana na watoa huduma wa afya katika kuhakikisha ubora wa takwimu unazingatiwa.
7. Kushirikiana na wadau/wafadhili katika kuboresha huduma kwa wateja wa CTC na huduma ya mama na mtoto.
8. Kushiriki katika kutoa elimu na ushauri nasaha kwa watu walio kwenye huduma za CTC.

9. Kuhudhuria mafunzo mbalimbali ndani ya Wilaya na Mkoa kama itakavyoelekezwa na Mkurugenzi au wafadhili.
10. Kufanya majukumu mengine kama atakayopangiwa na Mkurugenzi Mtendaji, Mganga Mkuu wa Wilaya na Mganga Mfawidhi wa Hospitali/kituo cha Afya/Zahanati

**MSHAHARA NA UKOMO WA MKATABA** – Kazi hii ni ya mkataba wa mwaka mmoja. Mshahara kwa mwezi ni Tsh. 700,000/=

Aidha maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, S.L.P. 320, Kyela.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **31.08.2017** saa **9.30 ALASIRI**.  
Watakaokidhi vigezo na kuchaguliwa kwa ajili ya usaili watajulishwa.

Imetolewa na:-

**Mussa J. Mgata**  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**  
**HALMASHAURI YA WILAYA,**  
**KYELA.**

---

Barua zote zitumwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Kyela